PRESS RELEASE

“UTALII UNAANZA NA MTANZANIA MWENYEWE”

MAONESHO YA BIASHARA YA UTALII WA NDANI YA KWANZA TANZANIA. TAREHE 15 HADI 17 FEBRUARY 2019 VIWANJA VYA MAKUMBUSHO YA TAIFA POSTA DAR ES SALAAM

UWANDAE EXPO 2019

Release imetolewa kwa ajili ya uzinduzi wa documentary ya kutangaza maonesho ya UWANDAE EXPO 2019 katika vyombo vya habari tarehe 15 January 2019

Wasiliana na:

Mary C. Kalikawe
Mwenyekiti
Association of women in Tourism Tanzania (AWOTTA)
(Waandaaji wakuu wa UWANDAE EXPO 2019)
Mob: 0759424933
Email: mkalikawe@gmail.com
Mob: 0718541751
E mail: kkts.tz@gmail.com

AWOTTA na washirika wake waamua kutekeleza mpango mkakati wa Bodi ya Utalii wa kuutangaza utalii wa ndani kwa vitendo
UWANDAE EXPO 2019
Kauli Mbiu ya Maonyesho haya ni: ***“Tambua ushindani wa Kibiashara katika Utalii wa Ndani Tanzania”.***

Sekta ya Utalii ni muhimili mkubwa wa uchumi na ustawi wa jamii duniani kote na hapa Tanzania pia. Watanzania tunahitaji tubadilike kiakili. Utalii sio kwenda kutembea mbuga za wanyama peke yake bali kuna utalii wa aina nyingi ikiwemo utalii wa Afya, Utalii wa michezo, wa mikutano, wa hija, utalii wa matamasha, kuona mambo ya ajabu, kujifunza, hata kutembelea ndugu na jamaa na mengineyo. Jumla ya gharama zilipwazo na wasafiri wa ndani wanaoishi humu humu Tanzania pamoja na mahitaji yao ya sehemu za kulala, chakula, malipo ya bidhaa na huduma walizozifuata huko walikoenda ndani ya nchi, zikiwekwa pamoja ni fedha kubwa sana yaweza kuwa hata mara tano zaidi ya fedha inayopatikana kutoka wasafiri wanaotoka nje au wale wanaokwenda kuona mbuga za wanyama peke yake (ILO na UN WTO).

Chama cha Wanawake katika fani ya Utalii Tanzania (AWOTTA) kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii (MNRT), Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Chama cha Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC), Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania(TanTrade) na shirika la maendeleo la Ujerumani GIZ, wameandaa documentary inayozinduliwa leo. Documentary hii inalenga kutoa mwanga na ladha ya maonesho ya Utalii wa ndani UWANDAE EXPO 2019 yatakayofanyika mwezi ujao mwezi wa February tarehe 15 hadi 17 katika viwanja vya Makumbusho ya Taifa (National Museum –Posta).

Kuzindua kwa documentary hii ikisisitiza mchango wa akina mama “ Nani kama mama” kunaenda sambamba na kuzindua matangazo kwa umma wa Tanzania juu ya uwepo wa sekta kubwa ya utalii humu nchini ambayo ni muhimu ikatambuliwa kusudi ihudumiwe na kupewa umuhimu wake. Sekta hii inachochea uwekezaji kwa wingi kama tunavyoona mahoteli, usafirishaji tangu wa ndege hadi wa bodaboda, biashara ya chakula kila pembe ya nchi, burudani na utalii wa aina nyingine nyingi. Sambamba na uwekezaji huu ,sekta ina uwezo mkubwa wa kutengeneza ajira kwa wakubwa na wadogo pia inabeba uwezo mkubwa wa kutengeneza kipato kwa mtu mmoja mmoja, makundi na kuchangia kipato cha taifa kwa kiasi kikubwa. Kwa sasa utalii wa mbuga za wanyama unachangia asilimia 17 ya pato zima la taifa ambayo ni takribani dolar Bilioni 2.1 au shillingi zaidi ya trillion 4.7 kila mwaka.

Taarifa ya tovuti https://www.nbs.go.tz/nbs/takwimu/Br/2014_15_SBR.pdf inaonesha takwimu zifuatazo: Kuwa mwaka 2014 jumla ya vitengo rasmi vya chakula vinywaji na malazi wakati huo Tanzania bara vilikuwa 11,136. Kati ya hivi asilimia 51.7 vilikuwa vya chakula na vinywaji wakati asilimia 48.3 vilikuwa ni sehemu za watu kulala.
Kwa upande wa sanaa na burudani, jumla ya vitengo rasmi katika utafiti wa mwaka 2014/15 vilikuwa 239 ambayo ni chini ya asilimia 1 ya vitengo vyote vya biashara vilivyotambuliwa mwaka huo. Kati ya hivi ubunifu na burudani vilikuwa

asilimia 35.6, michezo na starehe vilikuwa asilimia 24.3, michezo ya kubahatisha na kubeti ilikuwa asilimia 23.8 na vitengo vya library, kujisomea, makumbusho na burudani za utamaduni ilikuwa asilimia 16.3

Waandaaji wa maonesho wanapenda kutangaza kuwa kupitia uelewa wa upana wa sekta zilizomo katika utalii wa ndani, takwimu hizo hapo juu zimekwishaanza kubadilika na kupanda na mwamko wa watanzania na watoa huduma katika kuboresha utalii wandani utapandisha sana ukuaji wa vitengi hivi vya biashara.

Ni muhimu mikoa yote itambue umuhimu wa kuvuta wageni wa ndani kwenda kutembea kwa sababu mbali mbali katika mikoa yao. Kuwasili kwa wageni ndio ukuaji wa sekta ya utalii wa ndani. Takwimu hizo hapo juu zitajidhihirisha katika mikoa mbali mbali ikifanya bidii kuvuta wageni wa ndani na kuwapa huduma nzuri kama vile wanataka wageni wasahau kurudi kwao!

.
Maonesho haya yanatarajiwa kufunguliwa rasmi na **Mhe. Dr. Hamisi Kigwangala, Waziri wa Maliasili na Utalii** siku ya Ijumaa tarehe, 15 Februari 2019.
Lengo la Maonyesho haya ni kuanzisha utambuaji wa mapana ya sekta ya Utalii wa ndani na fursa kubwa za uwekezaji na ajira zinazoambatana na kukua kwa sekta hii muhimu. Maonyesho yatawaunganisha wafanyabiashara wa bidhaa na huduma katika maeneo mbali mbali yanayosababisaha safari za watanzania. Wafanya biashara hawa na vyombo vinavyowezesha uwekezaji, watatumia jukwaa hili kukuza uhusiano baina ya washiriki na Watembeleaji wa maonesho. Watu elfu tatu wanategemewa kuhudhuria maonyesho.
Faida ya kushiriki:
• Kuonyesha bidhaa au huduma wanazozalisha au wanazotoa;
• Kupata fursa ya kujifunza teknonolija mpya na ujuzi kutoka kwa washiriki wengine;
• Kupata fursa ya kushiriki katika kongamano na semina ya bure itakayofanyika sambamba na maonyesho hayo;
• Kukutana na Wafanyabiashara, Wawekezaji, washauri wa kibiashara na Wasambazaji wa huduma mbalimbali;
• Kupata kutangazwa kwenye utandawazi wa kitaifa na kimataifa kwa njia mbalimbali;
• Kupata fursa mbali mbali ambazo ni pamoja na tiketi ya raffle, vocha ya malazi, zawadi za kusafiri n.k.
Aidha, ni fursa ya kimkakati ya kuwahamasisha wananchi wa Tanzania kupenda kutumia huduma zinazotolewa na wadau wa sekta ya utalii hapa nchini.

Maonyesho haya yanatarajiwa kushirikisha, Wizara, Taasisi, Makampuni pamoja na Wafanyabiashara wa sekta mbalimbali. Kongamano litakuwa juu ya "Biashara, Uwekezaji na Ajira katika Utalii wa Ndani ambalo litatolewa bure (idadi ni watu 250 tu kwa siku moja wataruhusiwa,

hivyo jiandikishe mapema kabla nafasi hazijaisha).

Kiingilio kwenye maonesho ni bure asubuhi hadi saa 10 jioni. Kisha yanafuata masaa ya burudani ambayo inalipiwa kiasi kidogo.

Kwa mawasiliano zaidi tutafute:

Association of Women in Tourism Tanzania (AWOTTA)
House No.108/Plot 1334
Haile Selassie Road
Masaki, Dar es Salaam,Tanzania
Mobile: Mobile: +255 622 819 889/ +255 712 748 282/
+255 718 541 751
email: info@awotta.org
website: www.awotta.org